# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

## SALAMU ZA POLE



**Jaji Julie Catherine Manning**

**1939 – 2026**



Mkuu wa Chuo, Baraza, Menejimenti na Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) tumepokea kwa huzuni kubwa taarifa ya kifo cha Jaji Mstaafu Julie Catherine Manning kilichotokea tarehe 20 Machi 2026 katika Kituo cha Afya cha Hitech Sai, Upanga, jijini Dar es Salaam alipokuwa akipatiwa matibabu.

Jaji Julie Catherine Manning alizaliwa tarehe 24 Januari 1939 Mkoani Morogoro. Safari yake ya elimu ilianzia katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora kabla ya kujiunga na Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (kikiwa Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha London, Uingereza) mwaka 1961. Alikuwa mwanafunzi pekee wa kike miongoni wa wanafunzi 14 wa kwanza kabisa chuoni hapa, na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Tanganyika na Afrika Mashariki kusomea taaluma ya sheria katika chuo hiki.

Jaji Manning alihitimu Digrii ya Sheria mwezi Agosti mwaka 1964, akiwa miongoni mwa wahitimu 12 wa kwanza katika mahafali ya mwanzo kabisa katika Chuo hiki. Alianza kazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama mtaalamu wa uandishi wa sheria, akiwa mwanamke wa kwanza nchini kushika nafasi hiyo katika kipindi ambacho taaluma ya sheria ilikuwa ikitawaliwa zaidi na wanaume.

Mwaka 1973, aliteuliwa na Rais wa kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza Tanzania na Afrika Mashariki kushika wadhifa huo. Uteuzi huo uliashiria hatua muhimu katika historia ya maendeleo ya wanawake katika uongozi na taaluma ya sheria nchini na kanda ya Afrika Mashariki na Kati.

Jaji Manning aliteuliwa kuwa Mbunge mwaka 1975 na baadaye kuhudumu kama Waziri wa Sheria hadi mwaka 1983, akiwa miongoni mwa wanawake wa mwanzo kushika nafasi ya uwaziri kamili nchini Tanzania. Kupitia nafasi hiyo alitoa mchango muhimu katika kuimarisha utawala wa sheria katika kipindi cha awali cha ujenzi wa Taifa. Baadae alitoa mchango katika diplomasia alipohudumu kama mshauri wa masuala ya sheria katika Ubalozi wa Tanzania nchini Canada.

Jaji Manning vilevile alitumikia taifa katika nafasi mbalimbali za uongozi na ushauri, ikiwemo kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Parole kuanzia mwaka 1998, ambapo alishiriki katika kutoa mapendekezo ya msamaha kwa wafungwa waliokuwa na mwenendo mzuri. Aidha, aliwahi kuwa Kamishna asiye wa kudumu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa vipindi vitatu mfululizo hadi mwaka 2008, akishiriki katika kusimamia chaguzi za urais, ubunge na serikali za mitaa. Katika kipindi cha miaka kumi ya mwanzo ya utumishi wake katika Tume ya Uchaguzi, aliendelea kuwa mwanamke pekee katika tume hiyo, jambo lililodhihirisha zaidi nafasi yake ya kipekee kama kinara wa wanawake katika utumishi wa umma.

Kutokana na mchango wake mkubwa kwa taifa, mwaka 2011 alitunukiwa nishani ya heshima ya kitaifa na Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Aidha, katika maadhimisho ya miaka 50 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka huo huo, chuo kilimtunuku heshima kwa kulipatia jina lake moja ya mabweni ya wanafunzi, Julie Manning Hostel (zamani liliitwa Hall 3).

Kifo chake ni pigo kubwa kwa taifa na jumuiya ya taaluma ya sheria, kwani ameacha urithi wa uongozi, uadilifu, na kujitolea katika kujenga misingi ya haki na usawa, pamoja na kufungua milango kwa vizazi vya wanawake katika nafasi za uongozi. Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Jaji Julie Catherine Manning katika maendeleo ya taaluma ya sheria, utumishi wa umma na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Mkuu wa Chuo, Baraza la Chuo na Jumuiya nzima ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tunatoa pole za dhati kwa familia ya marehemu Jaji Julie Catherine Manning, ndugu, jamaa, marafiki, wanazuoni wa sheria pamoja na wote waliobahatika kufanya kazi na kujifunza kutoka kwake katika kipindi cha maisha yake.

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

**Imetolewa na**
**Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**
**21 Machi 2026**

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



Bakilana



El Kindy



Kakuba



Kaminwa



Kisse



Kivuitu



Kwikima



Manning



Miruka



Njenga



Ouma



Tibamanya

Hawa ni wahitimu 12 wa kwanza wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, katika Kitivo cha Sheria, waliotunukiwa Shahada ya Sheria na Mwalimu Julius Nyerere, Mkuu wa Chuo, kwenye Mahafali yaliyofanyika tarehe 21 Agosti, 1964.